# Kuweka mwenekano wa darasa kwa ajili ya wanafunzi wenye Uziwikutoona

Katika hali nyingi, wazazi na walimu hukutana na changamoto wanapojaribu kuwajumuisha watoto wenye Uziwikutoona katika shule za kawaida. Huenda wasijue jinsi ya kuwasaidia wanafunzi hawa darasani. Rasilimali hii itawasaidia kuelewa nini cha kufanya ili kuwasaidia watoto wenye ulemavu wa Uziwikutoona kuzoea na kujifunza vizuri zaidi.

a) Wape wanafunzi wenye uziwikutoona mwongozo kuhusu darasa na maeneo mengine kama maktaba, choo n.k. ili wajue mahali vilipo.
b) Panga vifaa vyote vya darasani katika eneo maalumu. Waambie/waonyeshe kila kifaa na eneo ili waweze kuvipata kwa urahisi.
c) Hakikisha kuna mwangaza wa kutosha darasani na hakuna kelele zitokazo nje au ndani ya darasa.
d) Hakikisha wanafunzi wenye uziwikutoona wanakaa kwenye siti/eneo la mbele. Itakuwa rahisi kwa mwalimu kuwasiliana nao. Mwalimu atazungumza kwa sauti ya juu kidogo na kuandika ubaoni kwa maandishi makubwa.
e) Tumia vifaa vya kujifunzia na vitu halisi inapowezekana.
f) Fahamu njia ya mawasiliano anayoipendelea mwanafunzi (lugha ya ishara, maneno, au lugha ya mguso) na wasiliana naye kwa njia hiyo.
g) Waelekeze wanafunzi wengine jinsi ya kuwasaidia wenzao wenye uziwikutoona.
h) Panga mikutano ya mara kwa mara na wazazi wao kuhusu maendeleo ya mtoto wao.